THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF EDUCATION AND CULTURE

FORM TWO SECONDARY EDUCATION EXAMINATION, 1993

0021

KISWAHILI

MUDA: Saa 2.00

1. Jibu maswali yote 13 katika karatasi za kujibia ulizopewa.
2. Fuata maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.
3. Kumbuka kuandika namba yako ya mtihani katika kila karatasi.

Karatasi hii ina kurasa 4 zenye maandishi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

## SEHEMU A - UTUNGAJI

1. Chagua kichwa kimoja cha habari kati ya hivi vifuatavyo na ukiandikie insha ya maneno yasiyozidi 200.

   (a) Umuhimu wa maji kwa maisha.

   (b) Uzuri wa mtu ni tabia.

2. Meneja wa Kampuni ya Kusindika Vyura S.L.P. 1203 DAR ES SALAAM ametoa tangazo katika gazeti la Uhuru tarehe 15.10.93 kuwa ana nafasi ya kazi ya uboharia. Andika barua ya maombi ya kazi hiyo.

## SEHEMU B UFAHAMU NA UFUPISHO

3. Soma habari hii kwa makini kisha jibu maswali yafuatayo:

"... Samaki ni chakula bora cha aina ya protini ambacho kazi yake ni kujenga mwili. Hivyo samaki ni miongoni mwa vyakula bora vinavyohitajika katika mwili wa binadamu. Katika samaki tunapata vitamini ambazo mtu akila hujipatia kinga za mwili wake ili asipatwe na ugonjwa wa kuvimba shingo. Umewahi kumwona mtu aliyevimba shingo chini ya kidevu karibu na koromeo? Ugonjwa huu, wataalamu wamegundua kwamba, unatokana na kukosa vitamini hizo. Aidha samaki hutupatia mafuta ambayo pia ni dawa. Kama macho yakipungua nguvu ya kuona, mgonjwa hupewa mafuta yake ambayo husaidia kutibu na kuilinda miili yetu.

Samaki pia hutumika kama chakula cha kuku. Unga wa dagaa huchanganywa na unga wa nafaka. Hiki ni chakula cha kufaa kabisa kwa malisho ya kuku (wa kisasa). Mifupa ya samaki pia husagwa na kutumika kama mbolea ya kurutubishia ardhi mashambani. Kazi hii ya kusaga mifupa siyo rahisi kwani haiwezi ikafanywa kwa mikono bali inahitaji mashine; hivyo inahitaji kufanyika katika viwanda maalum.

Katika maduka tunayo mikanda, mikoba na mapambo mengine ya nyumbani. Baadhi ya vitu hivyo hutengenezwa kutokana na ngozi ya samaki. Watalii wafikapo nchini hupendelea kununua vitu hivyo kwa wingi. Kiuchumi hutuongezea fedha za kigeni ambazo zinahitajika sana kwa uchumi na maendeleo ya taifa. Hivyo samaki hutuletea fedha ya ndani na za kigeni.

Siku hizi yapo mashirika ya mikoa na wilaya ambayo yameanzishwa kwa madhumuni ya kuimarisha shughuli za uvuvi na biashara ya samaki. Mashirika hayo hutoa ushauri juu ya njia mpya na za kisasa za kutumika katika uvuvi na biashara; njia ambazo zitawawezesha wavuvi wa Tanzania kujipatia samaki.

MASWALI

(i) Kwa sababu gani samaki ni miongoni mwa vyakula bora vinavyohitajika katika mwili wa binadamu?

(ii) Chakula cha kuku kitokanacho na samaki hutayarishwaje?

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

(iii) Kwa nini kazi ya kutengeneza mbolea hutokana na masalia ya samaki huwa ngumu?

(iv) Ni kwa vipi samaki hutuletea fedha za kigeni?

(v) Andika muhtasari wa habari hii kwa maneno yasiyozidi 100.

## SEHEMU C - SARUFI

4. Andika maana mbili kwa kila sentensi hizi:

   (a) Amechukua picha yangu.

   (b) Dada alinipiga kura.

5. Bainisha Kiima na Kiarifu katika sentensi hizi:

   (a) Yule mwimbaji maarufu aliyezawadiwa na Baba wa Taifa Mwalimu J.K. Nyerere amefariki.

   (b) Mtoto anayecheza pale ni mjukuu wake.

6. Ainisha sentensi zifuatazo:

   (a) Asingefanya uzembe angefaulu mtihani wake.

   (b) Juma ameondoka jana asubuhi.

7. Onyesha aina za maneno yanayounda sentensi hizi:

   (a) Baba aliamka kabla ya jua kuonekana.

   (b) Baba yake mdogo ni mfanyabiashara maarufu.

8. Bainisha viwakilishi vilivyopigiwa mstari:

   (a) Yangu haiandiki vizuri.

   (b) Upi ulitakiwa kufutwa kwanza?

## SEHEMU D - FASIHI SIMULIZI

9. Andika methali zenye maana karibu sawa na methali hizi zifuatazo:

   (a) Haraka haraka haina baraka.

   (b) Adhabu ya kaburi aijua maiti

   (c) Samaki mkunje yungali mbichi

   (d) Usisahau ubaharia kwa ajili ya unahodha.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

10 Soma kwa makini wimbo huu kisha jibu maswali yanayofuatia:

"Mwenzenu nifanyeje, nifanyeje jamani mie, ili na mimi nipate raha kama wengine. Kila nitendalo mimi mwenzenu sipati raha. Oh! nalilia raha, Oh! nalilia raha; raha siipati nifanyeje mie, tabu na mashaka ndiyo yanipatayo duniani."

MASWALI:

(a) Mwimbaji yuko katika hali gani?

(b) Wimbo huu una ujumbe gani?

(c) Ni jitihada gani mwimbaji anazifanya ili apate kufanikiwa?

(d) Lengo la mwandishi katika wimbo huu ni nini?

11. Taja sifa nne za ushairi wa fasihi simulizi.

12. Ili hadithi ya fasihi simulizi ikamilike ni lazima pawepo mambo manne. Yataje.

13. Jamii inapofanya matambiko inakusudia kufanya nini?

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner